



# WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI



## (RITA)

### TAARIFA KWA UMMA

#### **KUANZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA USAJILI NA KUTOA VYETI VYA KUZALIWA KWA WATOTO WA UMRI CHINI YA MIAKA MITANO KATIKA MKOA WA LINDI NA MTWARA.**

##### **1. UTANGULIZI:**

Ili kukabiliana na changamoto ya idadi ndogo ya Wananchi waliyosajiliwa na Kupata vyeti vya kuzaliwa (12.9% kwa mujibu wa Sensa ya Watu ya 2012), Serikali kupitia RITA imeanza kufanya maboresho ya mfumo mzima wa usajili kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Kuboresha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu (Vizazi, vifo, Ndoa na Talaka) na Takwimu [National Strategy on Civil Registration and Vital Statistics - kwa kifupi National CRVS Strategy)].

Mkakati wa CRVS una mipango mbalimbali ya utekelezaji ikiwa ya muda mfupi na mrefu kwa makundi yatokanayo na umri ili kufikia ufanisi unaotarajiwa. Makundi hayo ni la Watoto wa Umri chini ya miaka mitano, kundi la watu miaka 6- 18 na kundi la wananchi miaka 18 na kuendelea.

Utekelezaji wa Usajili kwa kundi la kwanza umeshaanza kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano ambapo kwa sasa umeshaanza na unaendelea kutekelezwa katika Mikoa saba ya Tanzania Bara ambayo ni Mwanza, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Geita na Shinyanga ambapo kwa ujumla watoto 1,606,703 wameweza kusajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

Misingi mikuu ya Mpango huu ni:

- i. Kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano bure ikiwa lengo ni kuhakikisha watoto wote ambao wazazi au walezi wao hawana uwezo nao wanapata haki yao ya msingi ya kutambuliwa. Vyeti vinavyotolewa katika mpango huu vinajazwa kwa mkono na ni halali kwa matumizi yoyote.
- ii. Huduma za usajili wa watoto kusogezwa karibu na maeneo ya wananchi hivyo huduma kupatikana katika Ofisi za Watendaji kata na katika vituo vya tiba vinavyotoa huduma za afya ya mama na mtoto.
- iii. Matumizi ya teknolojia kwa kutumia simu za kiganjani katika kuchukua na kutuma taarifa kwenda katika kanzidata ya RITA hivyo kusaidia utunzaji

(archiving) na upatikanaji (retrieval) wa kumbukumbu.

RITA inatekeleza Mkakati huu kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto Duniani (UNICEF), Serikali ya Canada kupitia Shirika Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Kampuni ya Simu za Mkononi ya TIGO.

## **2. KUANZA UTEKELEZAJI KATIKA MIKOA YA LINDI NA MTWARA**

Mwezi Septemba 2017, RITA inategemea kuanza utekelezaji wa Mpango wa Usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa katika halmashauri zote sita (6) za Mkoa wa Lindi na Halmashauri tisa (9) za Mkoa wa Mtwara .

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, ni asilimia 11.4 ya watoto wa Mkoa wa Lindi na asilimia 9.4 katika Mkoa wa Mtwara wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa. Lengo la RITA mara itakapoanza kutekeleza mpango huu ni kusajili watoto wote 281,270 ambao hawajasajiliwa na hawana vyeti vya kuzaliwa katika Mikoa yote miwili kwa kipindi cha miezi 6.

Ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huu kutakuwa na vituo vya usajili zaidi ya 797 vitakavyokuwa na wasajili wasaidiza wapatao 1594 kwa Mikoa yote miwili ambao watapewa mafunzo ya siku tatu ili kuwawezesha kutekeleza kikamilifu majukumu ya usajili. Vilivile kila kituo kitapewa simu ya mkononi iliyowekwa programu maalumu itakayowawezesha wasajili kutuma taarifa za watoto waliosajiliwa kwenda katika kanzidata ya RITA.

## **3. HITIMISHO**

Cheti cha kuzaliwa ni nyaraka ya awali ya utambulisho na inayomwezesha Mtoto kutambuliwa uwepo wake ambayo ni haki yake ya msingi. RITA inaamini itapata ushirikiano kutoka kwa wadau wote ikiwa pamoja na Viongozi wa Mikoa, wilaya, Halmashauri, Tarafa, Kata, Mitaa/ Vijiji na Vitongoji. Vile vile tunaamini tutapata ushirikiano kutoka kwa Viongozi wa Dini, Wanasiasa, Wanahabari na Viongozi wa jadi ambao watasaidia kuelimisha wananchi kuhusu Mpango huu.

Tunatoa rai kwa wananchi wote wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kutumia fursa hii kuwasajili watoto ambao wana umri chini ya miaka mitano mara Utekelezaji wa Mpango huu utakapoanza rasmi.

**Emmy Kalomba Hudson  
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu – RITA**

**Agosti 2, 2017**